HOTUBA YA MHE. Prof. MARK. J. MWANDOSYA (MB),
WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI
KWA WANANCHI WAKATI WA UZINDUZI WA MRADI WA MAJI WA MBAWALA CHINI KATIKA WILAYA YA MTWARA VIJIJINI
TAREHE 12.9.2009

Mheshimiwa Anatoly Tarimo, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara,
Mheshimiwa Erasto Mbwilo, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Vijijini,
Waheshimiwa Wabunge,
Waheshimiwa Madiwani,
Vyombo Mbalimbali vya Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Ndugu Wananchi,
Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kunipa heshima hii kubwa kuwa mgeni rasmi katika sherehe hii ya uzinduzi wa Mradi wa Maji wa Mbawala Chini. Kujumuika kwetu hapa kunaashiria umoja na ushirikiano mlionao katika kutatua masuala mbalimbali yanayohusu maisha yetu ya kila siku.

Ndugu Wananchi,
Serikali imeandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yenye lengo la kufanikisha upatikanaji wa maji kwa kiwango cha asilimia 65 kwa umbali usiozidi mita 400 na usafi wa mazingira kwa kiwango cha asilimia 95 kwa vijijini, ifikapo mwaka 2010.

Ndugu Wananchi,
Katika kufikia azma hiyo, katika Mkoa wa Mtwara, juhudi mbalimbali zimefanyika. Juhudi za hivi karibuni ni pamoja na ujenzi wa miradi ya maji ya visima virefu na chemchemi katika vijiji 31 uliofanyika kati ya mwaka 2003 na 2005 kwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan. Aidha, Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya *(European Union)* kupitia shirika la AMREF –Tanzania ilisaini mkataba wa maji na usafi wa

mazingira kati yake na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na shughuli ya uchimbaji wa visima imeshaanza. Mradi wenye thamani ya **shilingi bilioni tano** utahudumia jumla ya kata 6 za Halmashauri ya Mtwara Vijijini zenye jumla ya watu wapatao 60,000. Juhudi zingine ni kupitia *Tanzania Social Action Fund (TASAF)* mfuko ambao umegharamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maji.

Ndugu Wananchi,

Katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, kwa mwaka wa 2008/2009 miradi midogo ya ukarabati wa miundombinu imefanikisha ujenzi wa vituo vya kuchotea maji **132** vijijini. Kutokana na juhudi mbalimbali, hadi mwezi Desemba 2008, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kwa mkoa wa Mtwara ilikuwa asilimia 45.29 ikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa asilimia 58.3. Halmashauri ya wilaya ya Mtwara Vijijini inaongoza katika mkoa wa Mtwara kwa kuwa na huduma ya maji kwa asilimia 62.

Ndugu Wananchi,

Utekelezaji wa miradi mipya kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika mkoa wa Mtwara umekwishaanza kwa Mtaalam Mshauri kutafuta vyanzo vya maji na kufanya usanifu wa ujenzi katika vijiji 10 kwa kila halmashauri. Ili kufanikisha azma hii mikakati mbalimbali itatumika ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji; kuhamasisha wananchi kuhusu kuchangia mifuko ya maji na kuunda jumuia za kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Kampuni ya ushauri iliyoshinda ambayo ndiyo imekwishaanza kazi katika halmashauri zote za mkoa wa Mtwara ni *Don Consult Ltd* kwa kushirikiana na *Relief to Development Society (REDESO)* zote za Tanzania.

Ndugu Wananchi,

Sera ya Maji ya mwaka 2002 imeweka wazi kuwa wadau wote wanaruhusiwa kuchangia katika utoaji wa huduma ya maji nchini. Wadau wakuu ni wananchi wenyewe, Serikali, mashirika ya kidini, washirika wa maendeleo na sekta binafsi. Serikali inatekeleza Sera hiyo kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo asasi zisizokuwa za kiserikali zina mchango wake katika utekelezaji au uendeshaji wa miradi ya maji.

Ndugu Wananchi,

Kama mlivyoeleza kwenye taarifa ya mradi, Mradi wa Maji wa Mbawala Chini ulijengwa na kukamilika rasmi mnamo mwaka 1981 kwa ufadhili wa Serikali ya Finland kupitia shirika la *FINWATER* ukiwa unatoa huduma ya maji katika maeneo ya vijiji sita vya Kawawa, Nachenjele, Mbawala Juu, Naliendele, Mdui na Mkangala. Mradi pia ulikuwa unatoa huduma katika taasisi za zahanati ya Mbawala Juu, Shule za Msingi za Mbawala Juu, Nachenjele na Mbawala Chini na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele. Miundombinu ya skimu hii ilihusisha visima viwili, nyumba ya mashine na nyumba ya mhudumu wa mitambo, tanki kuu lenye meta za ujazo 200, tanki la kuchujia maji, matanki madogo ya chuma 6, magati 23 na pampu za kusukumia maji tatu.

Ndugu Wananchi,

Skimu hii ya maji ilisimama kufanya kazi mwaka 1991 kutokana na matatizo ya kuharibika kwa visima na pampu kukwama ndani ya visima hivyo. Baadaye uharibifu wa mabomba uliendelea kwani miundombinu hii ilikuwa haitumiki.

Mnamo mwaka 2007 kulipatikana mfadhili wa kusaidia kufanya matengenezo ya skimu hii ambaye ni Madame Navyn Saleem kwa kushirikiana na *Clinton Foundation HIV/AIDS Initiatives (CHAI)*. Matengenezo na ukarabati uliofanyika ni kama ifuatavyo:-

- Utafiti wa kihaidrojiolojia *(hydrogeological and geophysical survey);*
- Uchimbaji na uendelezaji wa visima virefu viwili kila kimoja chenye urefu wa mita 100 na kipenyo inchi; 6
- Ununuzi na ufungaji wa pampu za kuvuta maji *(submersible pumps)* mbili ndani ya visima, zenye uwezo wa kusukuma meta za ujazo 8 kwa saa kila moja pamoja na pampu ya kuongeza nguvu za maji *(booster pump)* yenye uwezo wa meta za ujazo 30 kwa saa;
- Ufyekaji wa njia za mabomba na ukarabati wa bomba kuu la maji lenye urefu wa kilometa 22;
- Ukarabati wa tanki kuu la kuhifadhia maji lenye meta za ujazo 200;
- Ukarabati wa matanki 7 ya kuhifadhi maji yenye ujazo tofauti
- Ukarabati wa nyumba ya kuhifadhi mitambo *(pump house)* pamoja na kuunganisha umeme kutoka Shirika la Umeme (*TANESCO),*

- Ukarabati wa magati ya maji na ukarabati wa mabomba ya kusambazia maji yenye urefu wa kilometa 3 pamoja na ufungaji wa dira za maji 32 katika vituo vya kuchotea maji.

Ndugu Wananchi,

Nimearifiwa kuwa mikutano ya uhamasishaji jamii ilifanyika katika vijiji vyote vya mradi, utoaji mafunzo kwa kamati za maji za vijiji kuhusu uendeshaji miradi ya maji, maudhui ya Sera ya Maji ya mwaka 2002, usomaji wa dira za maji, utunzaji wa vyanzo vya maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi na upandaji miti katika vyanzo vya maji pia imefanyika. Jumla ya **shilingi 202,125,000** zimetumika katika kukarabati mradi huu ambapo, shilingi 195,000,000 ni kutoka CHAI, shilingi 5,000,000 ni mchango wa Halmashauri na shilingi 2,125,000 ni thamani ya kazi za jamii (nguvu kazi). Kwa niaba ya Serikali, natoa shukrani kwa CHAI kwa kutoa mchango katika ukarabati wa mradi huu, mchango ambao pia ni wa kiwango cha juu.

Ndugu Wananchi,

Baada ya kukamilika kwa ukarabati wa mradi huu, huduma inatolewa kwa wananchi wapatao **19,066** katika vijiji sita, ambapo vinne ni vya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na vijiji viwili vya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani. Vijiji hivyo ni Kawawa, Nachenjele, Mbawala Juu na Mdui vya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na Naliendele na Mkangala vya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani. Mradi unao watumiaji binafsi *(private connections)* 6. Kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria ya Maji ya 2009, baada ya kukabidhi mradi huu kwa wananchi, ni jukumu la watumiaji wenyewe kusimamia uendeshaji na matengenezo kupitia vyombo ambavyo wamevichagua wenyewe na ambavyo vinatakiwa kusajiliwa kisheria.

Ndugu Wananchi,

Kufuatia maelekezo ya Sera ya Maji ya 2002 na Sheria ya Maji ya mwaka 2009, mchakato wa kuanzisha Chama cha Watumiaji Maji wa Mradi wa Maji wa Mbawala Chini ulianza tarehe 26.8.2008 kwa kufanya mikutano ya hadhara katika vijiji vyote vinavyopata huduma kutoka skimu hii. Katika mikutano hiyo wananchi wenyewe

walitakiwa kuchagua aina mojawapo ya Chombo cha Watumiaji Maji baada ya kuwezeshwa na wawezeshaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Vijiji vyote kwenye mradi vilikubaliana na uanzishwaji wa Jumuiya ya Watumiaji Maji Mradi wa Mbawala Chini *(Mbawala Chini Water User Association)*. Hadi sasa, mradi huu una jumla ya **shilingi 5,731,359** kwenye Benki. Aidha, Watumiaji Maji wameunda kamati ya utendaji katika kipindi hiki ambapo hati mbalimbali za zinazohusu uundaji wa jumuiya ziko ofisi ya Wizara yangu kwa hatua zaidi za kupitiwa na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali ili kuashiria uundaji rasmi wa Jumuiya.

Ndugu Wananchi,

Nimeambiwa kuwa Kamati ya utendaji ya Jumuiya ya Watumiaji Maji inaendelea na majukumu ya kuhakikisha kuwa huduma ya maji safi na salama inawafikia wananchi wote kwa usawa. Aidha, inafuatilia upatikanaji wa Hati ya Haki ya kutumia maji ya visima vile viwili kutoka ofisi ya Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini.

Ndugu Wananchi,

Changamoto zilizopo ni kuhakikisha kuwa mradi huu unaendelea kufanya kazi kwa kiwango cha sasa ili wafadhili na Serikali yenu iendelee kuwa na nia ya kusaidia miradi mingine. Natoa rai kwenu na kwa Taifa kwa jumla kuwa:

- Miradi yote ya maji iundiwe vyombo huru vya watumiaji maji. Kamati za maji ziwe ni ngazi ya kuunda vyombo hivyo.
- Vyombo vitakavyoundwa visajiliwe kisheria kulingana na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009. Vyombo hivyo vya watumiaji maji vijijini sasa vitasajiliwa kwenye Halmashauri husika badala ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kama ilivyokuwa huko nyuma.
- Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yana mchango mkubwa katika kutoa huduma ya maji vijijini. Hapa leo Mbawala Chini, jumla ya **shilingi 202,125,000** zimetumika katika kukarabati mradi huu. Huu ni ushahidi wa kutosha kuwa Sera ya Maji ya mwaka 2002 inatekelezwa na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kwa kuchangia katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi kama Sera inavyoelekeza.

Ndugu Wananchi,

Kwa kumalizia, natoa rai kwa mashirika yote, yale yasiyokuwa ya kiserikali (ikiwa ni pamoja na na mashirika ya kidini) pamoja na sekta binafsi, kuchangia katika kutoa huduma ya maji nchini. Serikali inathamini sana mchango wao. Kwa Mkoa wa Mtwara, mashirika ambayo yamechangia hivi karibuni ni pamoja na **CHAI, Action Aid International, Abasia Ndanda, Chingulungulu Mission, AMREF/EU, na TWESA WATER Finns.**

MAJI NI UHAI, NA USAFI WA MAZINGIRA NI UTU

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA